

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Barua pepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Lindi
19 Septemba, 2023

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RAIS SAMIA AAHIDI KUKABILIANA NA SUALA LA NDOVU KUSINI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amesema mkoa wa Lindi unakabiliwa na changamoto kubwa ya ndovu ambao huharibu mazao na kujeruhi wananchi.

Rais Samia amesema hayo wakati akihutubia mkutano wa hadhara mara baada ya kuweka Jiwe la Msingi kwenye ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Lindi iliyopo kijiji cha Mitwero.

Aidha, Rais Samia amesema Serikali inapanga mkakati wa kuanza kuifanyia kazi changamoto hii na kudhibiti ndovu ili kulinda usalama wa maisha na mali za wananchi.

Kuhusu migogoro ya wakulima na wafugaji inayokabili maeneo mengi nchini, Rais Samia amewataka viongozi kubuni mkakati wa kitaifa ili kutatua mgogoro huo.

Rais Samia pia ameweka Jiwe la Msingi mradi wa bandari ya uvuvi ya Kilwa Masoko inayotarajiwa kukamilika Februari 2025 kwa gharama ya shilingi bilioni 266 na kutoa ajira zaidi ya 30,000.

Vilevile, Rais Samia amezindua awamu ya kwanza ya ugawaji wa boti za kisasa ambapo jumla ya boti 160 za mkopo nafuu zitagawiwa kote nchini kwa ajili ya uvuvi na kilimo cha mwani.

Hali kadhalika, Rais Samia ameweka Jiwe la Msingi kwenye shule ya sekondari ya wasichana Lindi, iliyoko kijiji cha Kilangala ikiwa ni moja kati ya shule 10 zinazojengwa chini ya Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Sekondari (SEQUIP).

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

